// IMANI COLLEGE OF HEALTH AND ALLIED SCIENCE

P.O.BOX 100, SHIRATI – RORYA

Email: Imanicollage2016.health@gmail .com/info.ichas2019@gmail.com

Tel. +255763325826 /+255613200100 /+255763317089

**30th May ,2025**

**Kwa…………………………………………**

**YAH: KUJIUNGA NA MAFUNZO YA STASHAHADAYA UUGUZI NA UKUNGA KWA MWAKA WA MASOMO 2025/2026**

Napenda kuchukua nafasi hii kukupongeza na kukutaarifu kwamba Imani College of Health and Allied Sciences kwa kushirikiana na BarazalaTaifa la Elimu ya Ufundi na MafunzoyaUfundi Stadi (NACTVET) imekuchagua kujiunga na mafunzo Stashahada ya **Uuguzi na Ukunga** ngazi ya nne (NTA Level 4) katika Chuo cha **Afya na Sayansi Shirikishi cha Imani** Mafunzo haya ni Miaka Mitatu (3 ).

Chuo kitafunguliwa tarehe **10 Oktoba, 2025** na unapaswa kuripoti chuoni kuanzia saa 1.30 asubuhi hadi saa 11.30jioni. Endapo utashindwa kuripoti ndani ya wiki mbili hii nafasi yako itapotea na kujazwa na muombaji mwingine.

Ilikukamilisha usajili na kupokelewa chuoni unatakiwa kufanya yafuatayo:-

i) Kukamilisha malipo ya ada kama ilivyoainishwa katika majedwali ya gharama za mafunzo hapo chini.Malipo haya yatafanyika kupitia benki ya NMB tawi la Rorya Akaunti namba 32810010962, Imani College of Health na CRDB Tawi la Shirati 0150C788479700 SIYO KWA mitandao ya simu.
Mwanafunzi ambaye hatalipa ada iliyoainishwa kwenye Vipengele hicho hatapokelewa.

ii) Pima afya yako katika hospitali (sio zahanati/kituo cha afya) inayotambulika na kujaziwa Fomu ya Matibabu (MedicalExaminationForm) kabla ya kuripoti chuoni.

iii) KujazaFomuya Uthibitisho wa Utiiwa Sheria naTaratibu za Chuo utakayopewa ufikapo chuoni. Unakumbushwa kuzisoma na kuzielewa sheria zote kabla ya kusaini.

iv) Kujaza Fomu iliyoambatishwa hapo chini inayohusuTaarifa za Wazazi/Walezi wako

SEHEMU A: **MAELEKEZO YA MALIPO**

Kila mwanafunzi atapaswa kulipa Jumla ya**Tsh 2,350,400.00(Milioni mbilina laki tatu elfu hamsini na mia nne tu)** kwa mwaka (kwa wasio na BIMA ya Afya) naTsh 2,300,000.00 (Milioni mbili na laki tatu **tu)** kwa mwaka kwa walio na BIMA ya Afya kama gharama za mafunzo chuoni. Fedha **hizo zikishalipwa hazirudishwi (non-refundabIe).**

Mchanganuo wa malipo ni kama ulivyoainishwa katika majedwali yafuatayo:

**I.Gharama zinazolipwa moja** kwa moja Chuoni:

Malipo ya vipengele vifuatavyo yatalipwa moja kwa moja chuoni kwa kutumta namba ya AKAUNTI YA BENKI YA CHUO KAMA ILIVYOBAINISHWA HAPU JUU. Mwanafunzi anaweza kulipa malipo ya ada ya mwaka mzima kwa mara moja au kwa awamu mbili kama inavyoonekana katika mchanganuo ufuatao:

**UTARATIBU WA MALIPO YA KARO**

| Items | Semester 1 | Semester 2 | Total |
|---|---|---|---|
| **Tuition fee** | **855,000.00** | **795,000.00** | ***1,650,000.00*** |
| **Hospital's clinical Area practical** | **100,000.00** | **100,000.00** | ***200,000.00*** |
| **Internal exams** | **50,000.00** | **50,000.00** | ***100,000.00*** |
| **Maintenances and Recurrent Repairs** | **50,000.00** | **50,000.00** | ***100,000.00*** |
| **Student's development** | **10,000.00** | **10,000.00** | ***20,000.00*** |
| **Experience Book** | **25,000.00** | | ***25,000.00*** |
| **Delivery Case Book** | | **25,000.00** | ***25,000.00*** |
| ***PV BOOK*** | | **25,000.00** | ***25,000.00*** |
| ***KITAMBULISHO*** | **10,000.00** | **0** | ***10,000.00*** |
| ***JOZ MBILI ZA SARE*** | **100,000.00** | **0** | ***100,000.00*** |
| ***T-SHIRT*** | **15,000.00** | **0** | ***15,000.00*** |
| ***USAJILI MFUMO WA NACTVET*** | **30,000.00** | **0** | ***30,000.00*** |
| **GRAND TOTAL** | **1,245,000.00** | **1,055,000.00** | ***2,300,000.00*** |
| **OTHERS** | | | |
| **Double A Ream** | **1** | **1** | ***2*** |
| **Clean and Surgical Gloves** | **2** | **2** | ***4*** |

**Fedha zikishalipwa havirudishwi (non refundable).Malipo yafuatayo katika jedwali hapa chini SIYO SEHEMU YA KARO YA CHUO. Fika ofisi ya Mhasibu kupata MWONGOZO sahihi. Na malipo yote yafanyike mwanzoni mwa kila MUHULA .**

**MALIPO YA KARO YATAFANYIKA KWA AWAMU 3 (TATU) TU KAMA ILIVYOANISHWA HAPA CHINI KWENYE JEDWALI:**

| | S/N | MAELEZO | KIASI LIPWA | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| | 1. | KARO AWAMU YA KWANZA | 800,000.00 | 800.000.00 |
| | | | | |
| | 2. | KARO AWAMU YA PILI | 760,000.00 | 760,000.00 |
| | | | | |
| | 3 | KARO AWAMU YA TATU | 740,000.00 | 740,000.00 |
| | | | | 2,300,000.00 |

NB:

1.Malipo **tajwa hapojuu yanapaswa kufanyika** kila mwaka wa masomo.Ada ya **muhula** wa **kwanza awamu ya kwanza italipwa yote** mara **tu unapowasili chuoni na yamuhula wa pili italipwa ndani ya siku 14** baada ya kuanza muhula **wa pili.**

**SEHEMU B: MAHITAJI YA MWANAFUNZI AWAPO CHUONI**

Yafuatayo ni mahitaji muhimu ambayo mzazi/mlezi utapaswa kumuandalia mwanafunzi kabla ya kufika chuoni.

**I. SARE:**

**Wasichana:** Magauni mawili (2) ya rangi ya pinki yenye kola nyeupe (mshono/mtindo ataonyeshwa mwanafunzi akifika chuoni). Urefu wa gauni unaotakiwa ni ule unaopita magoti anapokuwa ameketi na pia magauni hayo yasiwe na ribbon/urembo. Viatu vyeusi vyenye kisigino kifupi kisichotoa sauti wakati wa kutembea sakafuni na soksi nyeupe. Nguo maalum kwa ajili ya kuvaa chumba cha upasuaji (theatre scrubs) rangi ya blue/kijani.

**Wavulana:** Suruali mbili (2) na mashati mawili yenye rangi nyeupe yenye rnikono mifupi na yasiyo na urembo (mshono/mtindo ataonyeshwa mwanafunzi akifika chuoni). Viatu vya ngozi vyenye rangi nyeusi na soksi nyeupe. Nguo maalum kwa ajili ya kuvaa rhumba cha upasuaji (theatre scrubs) rangi ya blue/kij ani.

**NB:** Mara utakapofika chuoni utapewa mwongozo wa mavazi wakati wote uwapo masomoni.

**IL VIFAA SAIDIZI KWAAJILI YA MWANAFUNZI**

a) Kifaa cha kupimia mapigo ya moyo (Stethoscope)

b) Kifaa cha kupimia msukumo wa Damu (BP Machine)

c) Kifaa cha kupimia joto la mwili (Thermometer)

d) Kifaa vya kupimia urefu (tape measure)

f) Vifaa vya kuandikia kwa mfano madaftari, kalamu, rula n.k

g) Nguo na viatu vya michezo mbali mbali.

i) Godoro (urefu wa futi tatu kwa sita)

k) Shuka nne (4) zenye rangi ya *light blue* kwa wavulana na *pink* kwa wasichana, mto mmoja na foronya mbili zenye rangi ya shuka, blanketi moja (1), chandarua na taulo **1**

**III. VIFAA SAIDIZI KWAAJILI YA CHUO**

a) 'Ream' moja ya karatasi za kutolea nakala/kudurufu (photocopy) kwa kila muhula kwa wanafunzi wanaoanza na wanaoendelea.

d) Picha nne (4) Passport size.

e) Examination/clean Gloves box 1 kwa kila muhula kwa ajili ya mafunzo ya vitendo wodini kwa wanafunzi wanaoanza na wanaoendelea.

Ninakutakia masomo mema.

_____________________________________

IMANI JORAM MBEBA

**MKUU WA CHU'.**

**Date:................................................**